


*BODABODA riders carrying passengers wait at traffic lights at the John Kijazi Interchange in Dar es Salaam yesterday. It has become common for both riders and passengers to travel without protective helmets, exposing themselves to serious safety risks. According to Muhimbili Orthopaedic Institute (MOI) neurosurgeon Dr Othman Kiloloma, seven out of every 10 bodaboda crash victims admitted to the institute suffer head injuries, largely due to failure to wear helmets. (Photo by Mohamed Mambo)*

GHARAMA ZA MAISHA

# Mafuta, usafirishaji vyapaisha bei ya sukari

Waandishi Wetu, Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

**Dar/mikoani.** Ongezeko la gharama za usafirishaji kutokana na kupanda kwa bei ya mafuta na mabadiliko kutoka kwa wasambazaji vimetajwa kuwa sababu za bei ya sukari kupanda katika mikoa mbalimbali nchini.

Hali hiyo imeongeza gharama za maisha na kupunguza uwezo wa wananchi kununua bidhaa hiyo muhimu.

Uchunguzi wa *Mwananchi* katika mikoa ya Simiyu, Geita na Tanga umebaini kuwa ongezeko la bei linatofautiana kati ya eneo na eneo kutokana na gharama za usafirishaji, kiwango cha mzigo uliopo kwa wafanyabiashara na mabadiliko ya bei kutoka kwa wasambazaji.

Mkoani Simiyu, kilo moja ya sukari kwa sasa inauzwa kwa Sh3,500 katika maeneo ya mijini na kufikia Sh3,800 vijijini, tofauti na bei ya awali ya Sh3,200 mijini na Sh3,500 vijijini kabla ya Julai mosi mwaka huu.

Mfanyabiashara wa sukari katika Mji wa Maswa, Gerald Justine, alisema kupanda kwa bei kumepunguza mauzo kwa sababu wateja wengi wamelazimika kupunguza kiwango wanachonunua.

"Wateja wengi wamepunguza kiwango cha sukari wanachonunua. Wengine waliokuwa wakichukua kilo tano sasa wanachukua kilo moja au mbili kutokana na kupanda kwa bei," alisema.

Mfanyabiashara wa Bariadi, Sophia Khija, alisema wao hawajapandisha bei kwa hiari, bali hulazimika kuuza kulingana na gharama wanazonunulia kwa wasambazaji.

Kwa upande wa wananchi, Frola Jilingisila wa Bariadi alisema ongezeko hilo limeongeza mzigo kwa familia nyingi zenye kipato cha chini, ambazo sasa zimeanza kupunguza matumizi ya sukari ili kuhimili gharama za maisha.

Mkoani Geita, kilo moja ya sukari ya kupima imeongezeka kutoka Sh3,200 hadi Sh3,500, huku sukari ya pakiti ikitoka Sh3,700 hadi Sh4,000, kutegemeana na eneo na bei ambayo mfanyabiashara alinunulia mzigo.

Mfanyabiashara wa Balenge, Wema Elias, anayeuza sukari kwa bei ya awali, alisema hali hiyo inatokana na muda ambao kila mfanyabiashara alinunua bidhaa hiyo.

"Sukari ya kupima nauza Sh3,500 kwa kilo na ya pakiti Sh3,700. Nilichukua mzigo mkubwa mwezi wa tano, hivyo nauza kulingana na gharama nilizonunulia," alisema.

Katika Mtaa wa Shilabela, mfanyabiashara Samson Idani alisema alianza kuuza sukari kwa Sh3,500 kutoka Sh3,200 kwa kilo baada ya gharama za usafirishaji kuongezeka kutokana na kupanda kwa bei ya mafuta.

Jijini Tanga hali si tofauti. Bei ya sukari imeongezeka kutoka Sh2,800 hadi Sh3,200 kwa kilo, huku wafanyabiashara wakisema mabadiliko ya mara kwa mara ya bei yanawatatiza wao na wateja wao.

Mfanyabiashara wa rejareja katika Barabara ya 17, Shedraki Yuseph, alisema mfuko wa kilo 50 umepanda kutoka Sh138,000 hadi Sh140,000 na kuwafanya wauze sukari kwa Sh3,200 kwa kilo badala ya Sh2,800.

Mfanyabiashara wa jumla katika Barabara ya 14, Haji Hamis, alisema waliambiwa uzalishaji wa sukari ya ndani ulipungua kwa kipindi fulani na kusababisha utegemezi wa sukari kutoka nje, lakini hata baada ya sukari ya ndani kurejea sokoni, bei imeendelea kuwa juu.

Kwa upande wake, mama lishe Aisha Mbwana, maarufu Mama Majuto, alisema ongezeko hilo limeongeza gharama za kuandaa vyakula na vinywaji kwa kuwa sukari ni kiungo muhimu katika biashara yake.

Akizungumzia suala hilo, Katibu Mtendaji wa Chama cha Wazalishaji wa Sukari Tanzania (TSPA), Kennedy Rwehumbiza, alisema hana uhakika wa kuwapo kwa mabadiliko ya bei kutoka kwa wazalishaji yaliyotangazwa hivi karibuni.

"Nitafuatilia nijue kama mabadiliko haya ya bei yameanzia kwa wazalishaji kweli au wasambazaji. Upande wa Zanzibar sisi hatuhusiki, kwani wanajisimamia wenyewe," alisema.